# Twende Pamoja

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Hutolewa kila baada ya Miezi Mitatu | Januari -Machi 2015 | Toleo Na 002



**Ndani**

Wanafunzi wasichana shule za Msingi na Sekondari kuanza kuvaa suruali Njombe. Uk.5

Shule za Msingi zajengewa vyoo vya Kisasa. Uk 6





**Habari katika picha Uk.7&8**


# 42,485 waandikishwa daftari la Kudumu la wapiga kura Njombe......Uk 4.




*Mkuu wa Mkoa wa Njombe Dr Rehema Nchimi aliyekaa wa tatu Kushoto akiwa na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Njombe wakati wa uzinduzi wa tuzo ya Mkuu wa mkoa.*



Mradi wa maji wenye thamani yaMilioni 200 wazinduliwa wiki ya Maji Njombe. 4



Kaya Masikini 5,307 Zatambuliwa Wilayani Njombe 5

## Tahariri

Karibuni wasomaji wetu katika toleo la kwanza la jarida la Twende Pamoja ambalo linatolewa na Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Kuanzishwa kwa jarida hili kunatokana na umuhimu wa wananchi kupata habari ikiwa ni haki ya msingi kwa jamii.

Halmashauri ya wilaya ya Njombe ikiwa inafanya kazi na jamii inawajibu wa kutoa habari kwa wananchi wake juu ya masuala mbalimbali.

Mbali na wajibu huo pia ibara ya 18 (d) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza wazi kuwa kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa kwa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Kwa kuzingatia matakwa hayo ya kikatiba Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeamua kuanzisha jarida hili ambalo litakuwa linatoka kila baada ya miezi mitatu.

Ili kutoa fulsa kwa kila mwananchi kuifahamu Halmashauri ya wilaya na shughuli inazofanya Jarida hili litakuwa likitoka kwa njia ya kawaida na pia litapatikana kwa njia ya mtandao (Online) kupitia mtandao wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe ambao ni www.njombedc.go.tz. Hii itatoa fulsa hata kwa Mtanzania aliyepo nje ya nchi kuweza kulisoma.

Ni matumaini yetu kuwa jarida litakuwa kiungo kizuri baina ya wananchi na Halmashauri na litaboresha mahusiano. Kupitia jarida hili wananchi wataweza kufahamu shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na Halmashauri pamoja na sera, mikakati na mipango inayofanywa na Jamii na Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Tunawatakia usomaji mwema na tutafurahi kupata maoni na ushauri ili kuweza kuliboresha jarida hili.

Sasa Twende Pamoja!

Linatolewa na Ofisi ya

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya

Njombe.

S.L.P 547 Njombe.

Phone: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email:ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti:www.njombedc.go.tz

## Shule za Sekondari na Msingi kubadilisha sare kukabiliana na Baridi.

Wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, mkoani Njombe watarajiwa kubadilisiwa sare tofauti na zile za awali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mabadiliko hayo ya sare yatahusisha Mkoa mzima wa Njombe ambapo kwa sasa wanafunzi wasichana wa shule za msingi na sekondari watavaa sketi na suruali kwa pamoja shati jeupe. Upande wa wavulana wa shule za Msingi na sekondari watavaa suruali na shati jeupe.

Kubadilishwa kwa sare hizo kunafuatia tafiti mbalimbali zilizofanywa katika maeneo kadhaa ya ndani na nje ya Mkoa wa Njombe ambako matumizi hayo yameleta mafanikio na hali ya afya kwa mwanafunzi.

Kupitia utafiti huo ilibainika kuwa hali ya hewa katika eneo kubwa la Mkoa wa Njombe ni baridi kwa kipindi kirefu cha mwaka inachangia kwa kiasi kikubwa kuathili afya pamoja na uboreshaji wa taaluma kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Tayari Halmashauri imeanza maandalizi na imeweka mikakati baada ya kupokea agizo kutoka kamati ya ushauri ya Mkoa wa Njombe (RCC).

Halmashauri ya wilaya ya Njombe ina jumla ya shule za sekondari 12 huku shule 10 zikiwa ni za serikali na mbili za binafsi.

zenye idadi ya wanafunzi 3479 na shule za msingi ziko 52 zikiwa na jumla ya wanafunzi 18,071.



# Wananchi 42,485 wameandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura

Jumla ya wananchi 42,485 wameandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura wakati wa uboreshaji wa daftari hilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mkoani Njombe.

Zoezi hilo limefanyika katika Kata 12 zilizoko Halmashauri ya Wilaya na lilianza Machi 6 hadi April 14 mwaka huu, kwa kutumia mfumo mpya wa Biometric Voters Register (BVR) limefanyika kwa ufanisi mkubwa katika Halmashauri ya Njombe.

Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura uliwahusisha wananchi wote waliokuwa na vitambulisho na wasiokuwa navyo ambao wamefikisha umri wa miaka 18 na kuendelea na ambapo watafikisha umri wa miaka 18 ifikapo wakati wa uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwezi wa kumi mwaka huu.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliweka lengo la kuandikisha watu 48,557 na kufanikiwa kuwaandikisha watu 42,485 sawa na asilimia 87.5 ya watu waliotakiwa kujiadikisha. Sensa ya watu na makaazi iliyofanyika mwaka 2012 ilibainisha kuwa Halmashauri ya Njombe ina idadi ya watu 86,103.

Jumla ya Kata 12 zilishiriki katika zoezi la uandikishaji na vijiji 45 huku idadi ya vituo vilivyotumika kwa ajili ya uandikishaji vikiwa ni 97. Hadi zoezi linakamilika hakukuwa na malalamiko ya watu kushindwa kujiandikisha kutokana na mashine kutofanya kazi kwa ufanisi au muda wa uandikishaji kuwa mdogo.

Mkoa wa Njombe ulikuwa mkoa wa kwanza kutumia mfumo mpya wa uandikishaji wa Biometric Voters Register ambao unahusisha uchukuaji wa alama muhimu za mtu ili kuweza kumtambua kilahisi.

Aidha katika zoezi hilo wananchi wameonyesha mwamko mkubwa wa kutumia haki yao ya msingi ambayo ni kupiga kura kuwachagua viongozi mbalimbali katika chaguzi zitakazokuwa zinafanyika.



*Afisa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Bw Dominic Mang'enyi akizungumza wakati wa kutoa mafunzo ya uandikishaji kwa Maopareta na waandishi wasaidizi.*



Waandishi wasaidizi na maopareta wa BVR wakiwa katika mafunzo katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

# Mradi wa maji wenye thamani yaMilioni 200 wazinduliwa wiki ya Maji Njombe.

Katika kuadhimishi wiki ya maji duniani Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Bi.Sarah Dumba ameweka jiwe la msingi kwenye mradi wa maji katika Kijiji cha Itambo Kata ya Mfriga wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 200 hadi kukamilika kwake.

Mradi huo umegharamiwa na shirika lisilo la kiserikali la Walemavu Nyombo kwa msaada kutoka shirika la Manos Unidas la Nchini Hispania, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe pamoja na wananchi wa kijiji cha Itambo.

Akizungumza na wananchi wakati wa kuweka jiwe la msingi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya, Bi.Anna Wiketye alisema kuwa mradi huo utawawezesha wananchi wa Kijiji cha Itambo kupata maji kwa umbali usiozidi mita 400 kwa mujibu wa Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002.

Bi.Wiketye aliongeza kuwa kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupunguza muda mwingi uliokuwa ukipotea kwa akina mama kufuata maji ambayo sio safi na salama kwenye milima na mabonde. Aliongeza kuwa kuwepo kwa mradi huo kutawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na kukuza uchumi wa kila mmoja.

Kwa upande wake Mhandisi wa maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Eng Sengayavene Mkalimoto aliwapongeza wananchi wa Itambo kwa kuunga mkono jitihada za Serikali na shirika la walemavu nyombo kupitia wafadhili kutoka Hispania katika kuwafikishia maji.

Mhandisi Mkalimoto aliwasisitiza wananchi wa Kijiji cha Itambo kuutunza mradi huo ikiwa ni pamoja na ku-



*Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengayavene S Mkalimoto akiangalia maji yanavyotoka baada ya mradi wa maji kijiji cha Itambo kuzinduliwa na Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Sarah Dumba katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya Maji wilayani Njombe.*

tunza vyanzo vya maji ili uwe endelevu kwa kutoa manufaa kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

Kwa upande wao wananchi wa Kijiji cha Itambo Kata ya Mfriga wameshukuru shirika la Walemavu Nyombo kuwasaidia kupeleka maji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe pamoja na wafadhili wengine.

Hadi sasa kazi zilizofanyika katika mradi huo ni ujenzi wa mtego, ujenzi wa njia kuu yeye umbali wa kilometa 10.9 pamoja na ujenzi wa chemba kwa ajili ya kutolea hewa. Kazi zingine ni chemba kwa ajili ya kutolea uchafu pamoja na tanki lenye ukubwa wa lita 45,000. Kwa sasa kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tanki la pili, kulaza bomba za kusambazia maji zenye urefu wa kilometa 5.1 pamoja na ujenzi wa vituo 19.

Mradi huu unafuatia ombi la kijiji cha Itambo kupatiwa ufumbuzi wa tatizo la maji ambap Halmashauri ya wilaya ya Njombe ilifanya uchunguzi wa awali na kuandaa gharama za mradi. Hadi sasa Shirika lisilo la Kiserikali la Walemavu Nyombo kupitia ufadhili wa shirika Kutoka Hispania

5



*Inatoka Uk...4*

la Manos Unidas wamechangia jumla ya shilingi milioni 119,096,000, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe shilingi milioni 58,000,000 na nguvu za wananchi ni shilingi 34,560,000.

Mradi wa maji Itambo utakapokamilika utaongeza idadi ya watu wanaopata maji safi na salama katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe na kufikia watu 46,805 kati ya watu 85,747 waliopa katika Halmashauri hii kwa mujibu wa sense ya watu na makazi ya mwaka 2012.



# Shule 12 za Msingi zajengewa vyoo vya Kisasa.



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Ninga wakinawa mikono baada ya kutoka choo . Choo hiki ni miongoni mwa vyoo vya kisasa ambavyo vimejengwa kwenye shule za Msingi za Halmashauri ya Wilaya Njombe.*

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa vyoo bora na vya kisasa katika shule 12 za msingi kupitia program ya afya na usafi wa mazingira shuleni (SWACH)

Ujenzi wa vyoo hivyo vya vya kisasa umezingatia miundombinu rafiki kwa watoto wenye ulemavu, chumba maalumu kwa ajili ya watoto wakike,sehemu ya aja ndogo kwa watoto wa kiume pamoja na kuwepo miundombinu ya unawaji mikono baada ya kutoka chooni.

Shule ambazo ujenzi wa vyoo vya kisasa umekamilika ni pamoja na shule ya Msingi Ninga, Lima, Ikondo, Ukalawa, Magomati, Mfriga,Upami,Wanginyi na Madeke pamoja na Image na Itunduma.

Aidha kwa sasa Halmashauri inaendele kutekeleza ujenzi wa vyoo bora na vya kisasa katika shule za Msingi Ikang'asi, Isitu, Lole, Idongela, Havanga,Lyalalo, Isoliwaya, kichiwa pamoja na Welela.

Sambamba na ujenzi wa vyoo hivyo vya kisasa Halmashauri inatoa mafunzo mbalimbali kwa wajumbe wa kamati za shule na waratibu elimu Kata,walimu wakuu pamoja walimu wa afya kwa shule zote zinazonufaika na program ya afya na Usafi wa mazingira mashuleni ili kuhakikisha kuwa miundo mbinu inayojengwa inakuwa endelevu.

Halmashauri ya wilaya ya Njombe ni miongoni mwa halmashauri nchini ambazo zinatekeleza program ya afya na usafi wa mazingira shuleni (School WASH program) . programu hii inahusisha ujenzi wa vyoo vya kisasa katika shule za msingi na inafadhiliwa na wadau mbalimbali wa afya ikiwemo UNICEF na Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii.

# Kaya masikini 5,307 zatambuliwa Njombe.

Mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya tatu umefanikiwa kutambua kaya masikini 5,307 wilayani Njombe.

Mpango huu unatekelezwa ili kujenga uwezo na kuziwezesha kaya masikini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitiaji muhimu pamoja na kuboresha maisha.

Utekelezaji wa mpango huo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambao ulizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dr Rehema Nchimbi ulianza mwezi januari mwaka huu ambapo lengo lilikuwa 4,733.

Ili kuutekeleza kwa ufanisi mpango huu warsha ya kujenga uelewa kwa wadau kuhusu mpango huu ilitolewa.Washa hii iliwahusisha wadau mbalimbali wakiwemo madiwani, wakuu wa idara na vitengo, kamati ya ulinzi na usalama, wawezeshaji ngazi ya Halmashauri pamoja na waandishi wa habari.

Aidha kwa sasa mchakato wa uandikishaji wa kaya masikini zilizokidhi vigezo unaendelea katika vijiji 44. Katika vijiji hivyo kaya 4,970 kati ya 5,307 zimekidhi vigezo sawa na asilimia 94.

Sambamba na mafanikio yaliyopatikana zipo changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa mpango wa TASAF awamu ya tatu. Changamoto hizo ni pamoja na mahudhurio hafifu katika mikutano ya vijiji hali inayopelekea zana ya mpango wa kunusuru kaya masikini kutoeleweka ipasavyo kwa wananchi.

Changamoto nyingine ni baadhi ya kaya maskini zilizotambuliwa kukataa kuingizwa kwenye mpango kutokana na imani za kidini, pamoja na walengwa kuhama katika maeneo yao ya awali.

Licha ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wameupokea kwa furaha mpango huu. Aidha viongozi wa ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na vijiji wametoa ushirikiano mzuri ili kufanikisha mapango huu.



*Wananchi wa Kata ya Mfriga Wilayani Njombe wakifanyiwa uhakiki katika utekelezaji wa Mpango wa kunusuru Kaya masikini unaotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia mradi wa TASAF awamu ya tatu.*

## Utafiti dhidi ya wadudu waharibifu wafanyika Kata ya Kichiwa.

Wataalam kutoka chuo kikuu cha Kilimo Morogoro (SUA),Syngenta na YARA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wamefanya utafiti wa namna ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao katika kijiji cha Ibumila Kata ya Kichiwa.

Utafiti huu unafuatia kuwepo kwa wadudu waharibifu wa mazao ambao kitaalamu wanaitwa White grubs na Kiswahili wanajulikana kwa jina la "Bungo" kuvamia na kuharibu mazao ya wakulima kwa kukata mizizi ya mahindi, maharage na alizeti katika Kijiji cha Ibumila Wilayani Njombe.

Matokeo ya utafiti unaofanywa yanatarajiwa kutolewa mwaka 2016 kutokana na utafiti kufanyika kwa kipindi cha misimu mitatu ya kilimo. Tayari umemefanyika katika msimu wa mwaka 2013/2014, 2014/2015 na 2015/2015.





*Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakifuatilia taarifa ya Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri kwa kipindi cha miezi mitatu katika kikao cha baraza la madiwani.*



*Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakiwa katika kikao cha baraza la ushauri la wilaya ya Njombe (DCC)*



*Wajumbe wa baraza la ushauri la Wilaya ya Njombe (DCC) wakifuatilia rasimu ya bajeti ya Halmashauri ya wilaya ya Njombe ya mwaka 2014/2014.*



*Wajumbe wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wakiwa na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya wakikagua chanzo cha maji kijiji cha Image*



*Kaimu afisa Maliasili Paulo Libenanga aliyenyosha mkono akitoa elimu juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kiwilaya katika Tarafa ya Lupembe kwenye chanzo cha maji Barazani*



*Wananchi wakishirikiana na wataalamu kupanda miti rafiki ya maji katika chanzo cha maji barazani Lupembe siku ya uzinduzi wa upandaji miti wilaya ya Njombe.*



*Wataalamu kutoka UNICEF wakikagua ujenzi wa vyoo vya kisasa ikiwa ni utekelezaji wa programu ya afya na usafi wa mazingira shuleni (SWACH) katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*



*Wataalamu kutoka UNICEF na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakikagua moja ya choo cha kisasa cha Mwananchi ikiwa ni utekelezaji wa Kampeni ya afya na usafi wa Mazingira Njombe.*



*Wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Sovi iliyopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe wakifanya mtihani fizikia kwa vitendo katika moja ya maabara zilizopo shuleni hapo.*



*Jengo la kisasa la maabara katika Shule ya Sekondari ya Lupembe ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali la kila shule ya Sekondari kuwa na maabara tatu za Kisasa.*



*Mkuu wa Mkoa wa Njombe (watatu kulia) akiwa na vongozi mbalimbali wakizindua tuzo ya Taaluma ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe katika viwanja vya Turbo Njombe Mjini.*





*Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya (mwenyesuti nyeusi) Sengayavene Mkalimoto akichota na kunywa maji na wanakijiji katika kuadhimisha wiki ya Maji Duniani.*